**KENYA NATIONAL PREDICTION TESTS**

# KCPE

# KISWAHILI
## SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

**NAMBA YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano:**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**22.** Barua ya kuomba kazi huitwa
   A. waraka
   B. barua maalum
   C. barua ya kiofisi
   D. Barua rasmi

Jibu sahihi ni **D**

**Katika karatasi ya majibu:**

[A] [B] [C] [D]   [A] [B] [C] [D]   [A] [B] [C] [D]   [A] [B] [C] [D]   [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **22**, kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

**Maswali 1 mpaka 15**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi **1** mpaka **15**. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo **zaidi** kati ya yale uliyopewa.*

Visa vya watoto kunyimwa haki zao ___**1**___ kupingwa kwa jino na ___**2**___. Hili lafaa kuchukuliwa kama jambo la dharura. Aidha, upo ___**3**___ wa jinsia baina ya watoto. Si ajabu kuwaona wazazi wakiwabagua watoto wao ___**4**___. Baadhi ya ___**5**___ wazazi huwadhamini watoto wa jinsia moja ___**6**___ lile jingine. Kwa sababu hii, upo umuhimu wa ___**7**___ jamii kuhusu umuhimu wa haki za watoto na jinsi ya kuwalinda watoto ___**8**___.

Watoto ndio nguzo katika jamii, nao wanajamii wote wana wajibu wa kuwalinda. Jukumu hili tusiliachie wazazi bali sote tuungane kwani ___**9**___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** zinapaswa | **B.** yanapaswa | **C.** inapaswa | **D.** vinapaswa |
| **2.** | **A.** ukucha | **B.** ulimi | **C.** unywele | **D.** upote |
| **3.** | **A.** dhuluma | **B.** ubaguzi | **C.** mateso | **D.** kunyanyaswa |
| **4.** | **A.** mwenyewe | **B.** zenyewe | **C.** wenyewe | **D.** yenyewe |
| **5.** | **A.** wawa hawa | **B.** wale hao | **C.** hawa wawa | **D.** hao huyo |
| **6.** | **A.** kuliko | **B.** kumliko | **C.** kukiliko | **D.** kuliko |
| **7.** | **A.** kuyaelimisha | **B.** kuihamasisha | **C.** kujifunza | **D.** kuitunza |
| **8.** | **A.** nyote | **B.** sote | **C.** zote | **D.** wote |

**9.** **A.** mwenye pupa hadiriki kula tamu **B.** aliyekupa kiti ndiye aliyenipa kumbi
**C.** kinga na kinga ndipo moto uwakapo **D.** joka la mdimu huwalinda watundao

Ulikuwa ni wakati wa ___**10**___ na umande ulikuwa dhahiri. Kila mmoja wetu alionekana akijitahidi ___**11**___ wajibu wake wa siku hiyo. Hata watoto hawakuachwa nyuma. ___**12**___ cha mikutano kilikuwa kimepambwa ___**13**__, hivyo basi kilionekana nadhifu. Mwendo wa ___**14**___, yaani mchana, sherehe ilianza kupamba moto kwani wageni walioalikwa walionekana ___**15**___ mmoja mmoja hadi mahali pa sherehe.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | **A.** macheo | **B.** magharibi | **C.** adhuhuri | **D.** mafungia ng'ombe |
| **11.** | **A.** kutelekeza | **B.** kuteketeza | **C.** kuteketea | **D.** kutekeleza |
| **12.** | **A.** Uwanja | **B.** Chumba | **C.** Jengo | **D.** Ukumbi |
| **13.** | **A.** kikapambua | **B.** kikapambikwa | **C.** kikapambika | **D.** kikapambwa |
| **14.** | **A.** jua mti kati | **B.** alasiri | **C.** jioni | **D.** asubuhi |
| **15.** | **A.** kutokomea | **B.** kufululiza | **C.** kulalama | **D.** kuchichiriza |

*Kutoka swali la **16** mpaka **30**, chagua jibu sahihi.*

**16.** Chagua jawabu ambalo si sahihi.
A. Kata ni kitendo cha kutokubaliana na jambo fulani
B. Kata ni eneo ndogo la uwakilishi
C. Kata ni kugawanya kitu katika vipande kwa kutumia kifaa chenye makali
D. Kata ni kifaa kinachotumiwa kutilia vitu viowevu

**17.** Geuza sentensi hii katika usemi wa taarifa:
Mhariri aliwaambia wanahabari,
"Tutakamilisha uandishi wa habari hizi leo."
A. Mhariri aliwaambia wanahabari kuwa watakamilisha uandishi wa habari hizo leo
B. Mhariri aliwaambia wanahabari kuwa watakamilisha uandishi wa habari hizo siku hiyo
C. Mhariri aliwaambia wanahabari kuwa wangekamilisha uandishi wa habari hizo siku hiyo
D. Mhariri aliwaambia wanahabari kuwa angekamilisha uandishi wa habari hizo siku hiyo

**18.** Nomino kutokana na kitenzi 'lipa' ni
A. mlipaji
B. kulipwa
C. lipiwa
D. mlifi

**19.** Chagua sentensi ambayo imetumia kihisishi.
A. Wakiwasili mapema watanipata nyumbani
B. Simile! Mpishe mama mwenye mzigo
C. Chausiku amekuwa kasuku darasani mwetu
D. Je, unamjua mtu huyu?

**20.** Ni aina ipi ya pambo ambalo huvaliwa sikioni?
A. Bali
B. Timbi
C. Mkanda
D. Ushanga

**21.** Maana ya semi 'kuenda masia' ni
A. kuenda bila mtu kujua aendako
B. kupitisha siku nyingi bila kula kitu
C. kutembea kwa miguu
D. kutembea kwa mwendo wa kasi

**22.** Geuza sentensi hii katika umoja;
Vyakula vyovyote vimepikwa vikaiva
A. Chakula zozote zimepikwa zikaiva
B. Chakula lolote limepikwa likaiva
C. Chakula chochote vimepikwa vikaiva
D. Chakula chochote kimepikwa kikaiva

**23.** Chagua sentensi iliyo sahihi kimantiki
A. Pale mlipoketi pana unyevu
B. Kule mlikoketi mna unyevu
C. Mle mlipoketi mna unyevu
D. Kule mlimoketi kuna unyevu

**24.** Andika tarakimu 20001 kwa maneno
A. Elfu ishirini na moja
B. Elfu ishirini na mia moja
C. Ishirini elfu na moja
D. Ishirini elfu na kumi na moja

**25.** Ni orodha ipi iliyo na viwakilishi pekee?
A. Njoo, ongea, keti, amua
B. Mimi, wewe, nyinyi, hawa
C. Nchini, shuleni, maegeshoni, nyumbani
D. Yule, gani, chake, wangu

**26.** Sentensi 'Asingalitia juhudi nyingi asingalifaulu,' ina maana kuwa
A. alitia juhudi nyingi japo hakufaulu
B. alifaulu kwa sababu hakutia juhudi nyingi
C. alitia juhudi nyingi na akafaulu
D. hakutia juhudi nyingi lakini alifaulu

**27.** Kamilisha majina ya makundi kwa usahihi
Msichana mwenye ____ la nywele amebeba ____ cha barua.
A. chane, kifurushi
B. korija, kitita
C. numbi, kikwaro
D. shungi, kipeto

**28.** Panga vifungu vifuatavyo ili kuunda sentensi sahihi kimaana:
*(i) uchafuzi wenyewe hufanywa na sisi binadamu*
*(ii) sharti sote tuwajibike katika kuyalinda mazingira*
*(iii) mazingira huwanufaisha binadamu na hayawani*
*(iv) ni kitendo cha aibu sana kuyachafua mazingira*

A. (iv), (iii), (ii), (i)
B. (iii), (iv), (i), (ii)
C. (ii), (i), (iii), (iv)
D. (iii), (i), (iv), (ii)

**29.** Chagua sentensi yenye kivumishi halisi
A. Mtoto mwingine amepokea tuzo
B. Vazi la Bi. arusi lilikuwa la chanikiwiti
C. Vikapu vivyo hivyo vimeletwa na wageni
D. Mbona wamdhulumu mtoto yatima

**30.** Sentensi 'bainika kama ardhi na mbingu' imetumia tamathali gani ya lugha?
A. Sitiari
B. Nahau
C. Takriri
D. Tashbihi

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **31** mpaka **40**.*

Kwa hali yoyote ile, binadamu huhitaji amani ili kuendesha shughuli zake kama vile inavyotakikana. Hakuna jambo lolote la manufaa ambalo linaweza kutokea katika mazingira ambayo hayana amani. Hivyo basi, yapo maana ya kukuza uwepo wa amani na utulivu katika maeneo ambayo tunaishi. Hili ni kwa sababu ukosefu wa amani na utulivu husababisha gharama kubwa ambayo haiwezi kulipika kwa urahisi. Aghalabu, watu hupoteza maisha yao, mali ya watu huharibiwa na vile vile haki za watu kukiukwa kwa kiwango kikubwa. Isitoshe, maendeleo katika maeneo yasiyokuwa na **amani hutoweka kama moshi**. Miradi yoyote ya maendeleo iliyokuwa imeanzishwa hapo awali hutumbukia nyongo.

Katika taifa letu, jamii zinazozozana ni kielelezo bora cha matokeo ya ukosefu wa amani maishani. Hapa petu nchini, kwa mfano, tatizo la wizi wa mifugo limeshamiri na kukita mizizi. Nazo athari zake huwa dhahiri miongoni mwa wanajamii wenyewe na taifa nzima kwa jumla. Kwanza, jamii zenyewe hulazimika kuhama maeneo yao hadi sehemu zenye amani. Wao huacha mali yao na katika hali ya kuhama, familia zao husambaratika. Upweke na ukosefu wa furaha na utulivu huzidi. Jamii zinazoshikilia uovu wa wizi wa mifugo humu nchini hushikilia dhana potovu kuwa hii ni njia murua ya kuchuma riziki isiyo na kifani. Wengi wanaotekeleza uovu huu huwa hawataki kuchoka au kumwaga jasho kwa lolote lile. Huu ni uzembe kwani kila mtu anapaswa kujua kuwa **mtaka la waridi sharti adhurike**. Isitoshe, mali ya mwenyewe haiwezi kutegemewa kamwe kwani hii ni nguo ya kuazima. Sharti kila mtu awe tayari kufanya kazi ili apate ufanisi.

Ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana ni changamoto kubwa sana hapa nchini. Wanapokosa gange, vijana wengi huingilia vitendo hasi kama vile wizi wa mabavu na ukahaba, vitendo ambavyo huvuruga amani katika jamii. Inashangaza sana kuona jinsi vijana wanavyotumiwa na wanasiasa kuzua uzushi. Wanapoitisha mikutano wanasiasa hawa, vijana huhudhuria mikutano hii kwa wingi, jambo linaloonyesha kuwa vijana wengi huwa hawana kazi ya kufanya. Kupitia mikutano hii, wanasiasa hupata nafasi ya kufukia mbegu ya uhasama, ukabila na chuki kwa matamshi yao. Badala ya kuhubiri amani, wao huvuruga amani ambayo tayari imekuwa ikisheheni. Wanasiasa kama hawa wanapaswa **kula kalenda** kwa maovu yao. Vile vile, vijana wanapaswa kushauriwa dhidi ya kufuata ushawishi wa viongozi usioleta manufaa kwao. Waweze kuwa na akili ya kujua mazuri na mabaya yanayohubiriwa na wanasiasa hawa. Nayo serikali inapaswa kuunda nafasi za ajira ili kukidhi mahitaji ya vijana, jambo ambalo litasaidia kupunguza uovu unaotekelezwa na vijana. Vile vile, lazima kila mtu awe tayari kufanya kazi yoyote bila ya kuwepo kwa ubaguzi wa kikazi. Watu wengi, hasa vijana hubagua kazi. Vijana wengi hupenda kufanya kazi za kiofisi au za starehe zisizohitaji nguvu nyingi kwani hawapendi kuchoka. Hata hivyo, kazi hizi huwa ni chache mno na mara nyingi zimeadimika kama wali wa daku. Hivyo basi, vijana wengi hubakia bila ajira.

Ili kukuza amani katika jamii, sharti maadili kama vile upendo, kufanya kazi kwa bidii na utangamano yakuzwe miongoni mwa wanajamii. Aidha, usawa wa makundi yote katika jamii lazima uhimizwe, hivyo basi maskini ama walemavu wasipuuzwe katika jamii. Mwishowe, lazima tofauti za kisiasa, kikabila na kimaisha zitupwe katika kaburi la sahau.

**31.** Katika mstari wa kwanza, mwandishi anatoa dhana kuwa
A. kila binadamu huendesha shughuli zake jinsi inavyotakikana
B. uendeshaji wa shughuli za binadamu unahitaji amani
C. ni vigumu kwa binadamu kuendesha shughuli zake jinsi inavyotakikana
D. amani huhitajika kwa kiasi kidogo na binadamu.

**32.** Ni yapi si madhara yatokanayo na ukosefu wa amani?
A. Kutofaulu kwa miradi ya maendeleo.
B. Uharibifu wa mali ya watu.
C. Uboreshaji wa hali ya maisha.
D. Ukiukaji wa haki za binadamu.

**33.** Maneno 'amani hutoweka kama moshi' yametumia tamathali gani?
A. Tanakali.
B. Nahau.
C. Tashbihi.
D. Methali.

**34.** Uovu wa wizi wa mifugo huchangiwa pakubwa na
A. kuwepo kwa nafasi nyingi za ajira
B. uimarishaji wa maadili katika jamii
C. watu kutaka kutoa jasho ili kuchuma riziki
D. tamaa ya watu ya kutaka kupata utajiri kwa urahisi.

**35.** Methali 'mtaka cha waridi sharti adhurike' katika taarifa limetumiwa kuhimiza
A. umuhimu wa kutia juhudi ili kupata ufanisi
B. umuhimu wa utangamano katika jamii
C. manufaa ya kutobagua kazi miongoni mwa vijana
D. ukomeshaji wa vitendo viovu miongoni mwa vijana.

**36.** Idadi kubwa ya vijana wanaohudhuria mikutano inayoitishwa na wanasiasa inaonyesha kuwa
A. vijana wengine humu nchini ni wazalendo
B. vijana wengi ni wasikivu wanaopenda kurekebishwa
C. vijana wengi hupenda kurandaranda ovyo ovyo
D. idadi kubwa ya vijana haina ajira

**37.** Maana ya semi 'kula kalenda' kam ilivyotumika katika taarifa ni
A. kukosa gange
B. kufungwa jela
C. kula kwa pupa
D. kukosa jambo ulilolitarajia.

**38.** Kwa mujibu wa taarifa, vijana wengi hubagua kazi kwa sababu
A. huwa hawapendi kazi zinazowachosha
B. huwa hawapendi kazi za kiofisi kamwe
C. ni haki yao kufanya kazi yenye hadhi
D. wao hupenda kazi za kijungu jiko.

**39.** Mwandishi anashauri mambo yafuatayo yatekelezwe ili kukuza amani ila
A. kuimarisha utangamano katika jamii
B. kuimarisha hali ya juhudi kazini
C. kupuuza walemavu katika jamii
D. kutupilia mbali tofauti za kisiasa na kikabila.

**40.** Kichwa ambacho kingefaa kuelezea taarifa hii zaidi ni kipi?
A. Ukosefu wa ajira miongoni mwa wanajamii.
B. Umuhimu wa kuimarisha amani katika jamii.
C. Udororaji wa maadili miongoni mwa vijana.
D. Tatizo la wizi wa mifugo humu nchini.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **41** mpaka **50**.*

Siku yenyewe ilipotimia nikiwa buheri wa afya, nilimrudishia Mola shukrani zisizo haba. Ilikuwa ni siku ambayo mimi pamoja na nyanya yangu aliyekuwa amebugia chumvi ya kutosha tungeenda mjini. Nyanya alitaka kumtembelea mjukuu wake, Karisa, ili apate matibabu kwani alikuwa anaugua. Uwele ulikuwa umemfanya aonekane dhaifu na asiye na siha njema. Basi asubuhi hiyo, baada ya kufanya matayarisho yaliyohitajika, **nilimpa mziwanda wangu mkono wa buriani**. Hakusahau kunituma salamu kwa Karisa, ambaye ndiye aliyekuwa kifungua mimba katika familia yetu. Niliandamana na bibi hadi kwenye kituo cha mabasi.

Tulisuburi pale kwa dakika kama ishirini hivi kabla ya matwana moja kufika stanini. Bila kuwa na fikira zozote, tulijitoma mle ndani huku tukitarajia kufika mjini salama salimini. Katika muda wa kupiga ukope, daladala ile ilijaa watu mithili ya siafu na muda si mwia, safari yetu ikang'oa nanga huku kila mmoja wetu akionekana kuwa mchangamfu. Nyanya alikuwa amesheheni uchangamfu mwingi. Kwa muda wa dakika chache, gari liliondoka pale stanini. Mwendo wenyewe ulikuwa ni ule wa kasi. Ndani ya gari, watu walirushwa kutoka upande mmoja hadi ule mwingine. Licha ya hayo, mifugo waliokiwa wamejazwa pale garini wote walilalamika kwa maumivu. **Hata nafasi ya kutema mate haikuwa**. Isitoshe, muziki ulidunda na kuhinikiza dududu kama baruti katika machimbo ya mawe. Watu walilalamika kuhusu jambo hilo, lakini ole wao! Dereva mwenyewe alionekana katia komango masikioni. Waama, sikio la kufa halisikii dawa.

Kila mmoja wetu alishikilia roho mikononi huku akimwomba Maulana afike salama. Hata mimi mwenyewe sikuwa na wakati wa kujionea mandhari, jambo ambalo nililipenda sana. Nilijaribu kumsihi dereva apunguze mwendo lakini hilo lilikuwa ni kama kujenga nyumba ya karatasi. Nilivyoona hivyo, basi niliamua kutupa jongoo na mti wake. Usingizi nao ulinipata, lakini singeweza kulala vizuri kwa sababu ya makelele yaliyosheheni mle ndani ya gari. Dereva mwenyewe alijawa na tamaa, hata akaamua kuiendesha gari hilo kwa mwendo wa juu. Ya wahenga kuwa haraka haraka haina baraka yalimpaa akilini. Kondakta naye alikuwa mtukutu ja mkia wa mbuzi. Aliitisha nauli kutoka kwa wasafiri kwa njia isiyo na heshima. Alibweka na kutoa maneno ya matusi, bila kuzingatia aliyonena.

Tulipita milima na mabonde huku gari likidanadana kama mpira. Tulitarajia kufika mjini mwendo wa jua la utosini. Hata hivyo, hilo halikuwa litimie, ndiposa wahenga wakasema ya kwamba usimkatie mtoto kanzu kabla hajazaliwa. Takriban kilomita kama ishirini hivi kutoka mjini, jambo ambalo halikutarajiwa lilitokea. Niliusikia mlipuko mkubwa kama wa bomu. Kutanabahi, damu ilikuwa imetapakaa kote barabarani. Viwiliwili vya watu vilikuwa vimeanguka mahali pa ajali na maeneo yaliyokuwa karibu na eneo hilo. Ama kweli, waliosema kuwa ajali haina kinga wala kafara hawakukosea.Nilijaribu kuangaza angaza pale na pale nitafute nyanya yangu, licha ya kuwa pia mimi nilikuwa nimeumia. Nilipomwona nyanyangu, moyo wangu uliatuka. Nyanya alikuwa akibebwa na wahisani waliokuwa wakiwaingiza manusura katika gari la ambulensi. Nyanya mwenyewe alikuwa si wa maji si wa uji. Hata mimi niliwekwa ndani ya gari hilo. Hatimaye, tulipelekwa hospitali kuu. Tulilazwa hapo kwa siku ayami huku tukiendelea kupokea matibabu. Ama kweli, lisilo budi hubidi.

**41.** Mwandishi alitoa shukrani kwa Rabana kwa sababu
A. siku ya safari ilitimia
B. alikuwa na pesa za masurufu
C. angesafiri hadi mjini
D. alikuwa mwenye siha njema.

**42.** Madhumuni ya mwandishi na bibiye kuenda mjini yalikuwa ni yapi?
A. Nyanya alisisitiza kuzuru mjini.
B. Nyanya alitaka kumsabahi mjukuuwe.
C. Nyanya alikuwa muwele hivyo basi alihitaji kupata matibabu.
D. Nyanya alikuwa amebugia chumvi ya kutosha.

**43.** Maneno 'nilimpa mziwanda wangu mkono wa buriani' yanamaanisha kuwa
A. mwandishi alimuaga mdogo wake
B. mwandishi alimtahadharisha mdogo wake
C. mwandishi alielekea upande aliokuwa mdogo wake
D. mwandishi alitumwa salamu kwa nduguye Karisa

**44.** Matarajio ya mwandishi na nyanya yake baada ya kuabiri gari yalikuwa
A. kula vya unono kwa Karisa mjini.
B. kufika mjini katika hali nzuri.
C. kupata watu wenye roho za utu mjini.
D. kupata matibabu ya haraka huko mjini.

**45.** Ni nini kinaonyesha kuwa nyanyake mwandishi alifurahia safari ile?
A. Alikuwa na hamu ya kufika mjini.
B. Gari lenyewe lilikuwa limejaa watu kupita kiasi.
C. Alikuwa amejawa na uchangamfu.
D. Gari liliondoka pale stanini bila kubanaga wakati.

**46.** 'Hata nafasi ya kutema mate haikuwa.' Kwa kusema hivi, mwandishi anamaanisha kuwa
A. kulikuwa na nafasi pale ndani ya gari kiasi cha mtu kuweza kutema mate
B. sauti ambayo ilikuwa imefunguliwa ilikuwa ya kuharibu masikio
C. ilikuwa vigumu watu kupumua kwa sababu walipitia juu ya machimbo ya mawe
D. idadi ya watu waliokuwa ndani ya gari ilikuwa kubwa.

**47.** Baada ya wasafiri kulalamika, ni sahihi kusema kuwa
A. dereva alijitia hamnazo asijali la mwadhini wala la mteka maji msikitini
B. wasafiri walikataa kutoa pesa za nauli
C. dereva aliitikia kufuata wasia wa wasafiri
D. dereva alikerwa sana na kusitisha mwendo.

**48.** Kwa nini mwandishi hangeweza kulala ndani ya gari?
A. Alikuwa yu macho akimlinda nyanya yake.
B. Muziki uliohinikiza ndani ya gari ulitatiza utulivu.
C. Alitaka kujionea mandhari ya pale barabarani.
D. Alitaka awe macho endapo ajali ingetokea.

**49.** Ni jambo gani linaloonyesha utukutu wa kondakta katika taarifa?
A. Kuwalipisha wasafiri nauli maradufu.
B. Kutomuasi dereva dhidi ya mwendo wake wa kasi.
C. Kudai nauli kutoka kwa wasafiri kwa njia isiyo ya heshima.
D. Kwa kuendesha mwendo wa kasi kwa sababu ya tamaa.

**50.** Ni kauli gani si sahihi kulingana na taarifa?
A. Gari lilihusika katika ajali kabla ya kufika mjini.
B. Nyanya alikuwa katika hali mahututi baada ya ajali.
C. Mwandishi na nyanyaye walilazwa siku nyingi hospitalini.
D. Mwandishi na nyanyaye walirudisha nyusi kwa Muumba.